# MWONGOZO WA MAOMBI

kwa Conférence Générale ya Kanisa Méthodiste Unie

Imetayarishwa na wafanyakazi wa
THE UPPER ROOM®



...and KNOW that I am GOD

The United Methodist Church General Conference | CHARLOTTE, NORTH CAROLINA

# MWONGOZO WA MAOMBI

## kwa Conférence Générale ya Kanisa Méthodiste Unie

### Imetayarishwa na wafanyakazi wa The Upper Room

Copyright © 2024 kwa The Upper Room, Inc. 1908 Grand Ave., Nashville, TN 37212-2129, U.S.A. Haki zote zimehifadhiwa.

Couverture ya kitabu na McKenzie Baker
Picha na Paolo Nicolello

Jiandikishe ku kitabu ya méditations ya The Upper Room kwa kuchapishwa au dijitali katika **UpperRoom.org/subscribe**.

Pata maelezo zaidi kuhusu matoleo mbalimbali ya lugha ya The Upper Room katika **UpperRoom.org/international**.

---

Nukuu za Maandiko zenye alama BHN zimechukuliwa kutoka kwa Biblia Habari Njema

## Mfano wa kutumia kitabu

**Mbele ya kuanza:** ikala kimya kwa sekunde 30 ili kutuliza akili yako. Kupumua na pumzika.

**Soma:** Fungua Biblia yako na usome sehemu ya andiko iliyopendekezwa chini ya kichwa.
Baada ya kusoma, tulia ili kufikiria maandiko. Nini kinakuja ku akilini? Ni nini kilikuvutia macho yako?

**Mstari wa Biblia:** Mstari uliotajwa inahusu sehemu kuu ya ibada. Isome polepole na ufikirie maana gani kwako. Mara moja au mbili kwa juma unaweza kukariri mstari wa Biblia.

**" Historia":** Ibada zimeandikwa kwa watu kutoka duniani kote. Baada ya kusoma sehemu kuu, jiulize, "jinsi gani neno hili ina ungana na maisha yangu?"

**Maombi:** Ili kumaliza muda wako wa utulivu, omba ombi chini ya page. Unaweza kuongeza, ukitaja watu au hali zinazokuja akilini wakati huo.

**Mawazo ya Siku:** Hii inakualika kujibu au kutoa mawazo ya kusoma kwa siku. Rudia wazo hili mara chache na ulikumbuke siku nzima ili kujikumbusha yale uliyosikia kutoka kwa Mungu.

**Kusudi ya Maombi:** Hili linapendekeza somo la kuendelea na maombi baada ya muda wako wa ibada, kuunganishwa na waumini duniani kote.

**Ukiwa na kikundi:** Tumia hatua zilizoainishwa hapo juu na kikundi. Uliza mtu asome kwa sauti swali ya siku hiyo la ibada. Mpe kila mtu nafasi ya kujibu. Zungumza juu ya kile ambacho kila mtu anafikiri, na jaribu kusikia kile ambacho Mungu anaweza kusema kwako.

# Neno la kukaribisha

Mada ya Conférence Générale ni “ . . . **nanyi mjue ya kuwa mimi ni Mungu.**” Ili kuwatayarisha kwa safari, tunatoa mwongozo huu wa ibada kama njia ya kuimarisha ujuzi wako wa Mungu.

Tunawezaje kumjua Mungu kweli? Kumjua Mungu huanza na kuwa katika uhusiano na Mungu, Yesu, na Roho Mtakatifu. Tuna pata ujuzi wa Mungu kwa njia nyingi - kupitia watu, hali, ulimwengu, ibada, muziki, na maombi - hiyo ni mifano michache tu. Maudhui ya mwongozo huu yameandikwa na watu kutoka duniani kote ambao wamepata uwepo wa Mungu katika nyakati za kawaida katika maisha yao. Uzoefu wao inatupa mitazamo mipya ya jinsi Mungu anavyofanya kazi ulimwenguni. Tunatumainia kwamba mwongozo huu wa ibada itakongoza katika mawazo tulivu, yaliyo wazi tunapokusanyika kufanya kazi ya kanisa. Tukumbuke si kuhusu ajenda zetu lakini ni kile Mungu na Roho Mtakatifu wanaweza kufanya ndani yetu na kupitia kwetu kwa ajili ya tengeneza kanisa zima kwenye Conférence Générale.

Haijalishi kule tunatoka, maombi inaweza kutuunganisha wote katika misheni yetu moja ya kutofanya mabaya, kutenda mema, na kukaa katika upenda na Mungu ( Kanuni za Jumla za Kanisa Méthodiste Unie. Bila kujali lugha yetu, msimamo wetu wa kimwili, au namna ambayo tunaomba, tunapaza sauti zetu katika maombi ya matumaini ya umoja, utume, na huduma kupitia Yesu Kristo kwa ajili ya kanisa letu.

Labda unafahamu mwongozo wa ibada ya kila siku ya *The Upper Room* (Chumba cha Juu), lakini tunaomba kwamba kutumia kitabu iyo kwa namna mpya ambao unapojitayarisha kwa ajili ya Conférence Générale italeta njia ya kumjua Mungu zaidi. Tunawashukuru wafanyakazi wa The Upper Room kwa mwongozo huu.

Sisi zote ni watoto wa Mungu na tuko ya thamani machoni ya Mungu. Kila mtu ule anakuwa ku mkutano huu ni mshiriki muhimu ya kanisa, mwili ya Kristo. Tuonyeshe heshima kwa kila mmoja wetu wakati huo tuko pamoja katika maombi na matayarisho.

— Kim Simpson
Mwenyekiti wa Tume ya
Conférence Générale

# PICHA KAMILIFU

**SIKU YA JUMA**
**07/04/2024**

**SOMA Zaburi 139:13-18**

***Wewe umeniumba, mwili wangu wote; ulinitengeneza tumboni mwa mama yangu. Nakusifu maana nimefanywa kwa namna ya ajabu, matendo yako ni ya ajabu; wewe wanijua kabisakabisa.***

**— Zaburi 139:13-14 (BHN)**

Niko katika harakati za kuchapisha kitabu changu cha kwanza. Ni kuhusu uzoefu wangu wa kudhulumiwa nikiwa mtoto kwa sababu nina kigugumizi. Picha yangu na wasifu wangu itakuwa kwenye jalada la nyuma. Maswali machache yanapita kichwani mwangu. Nivaeje nywele zangu ? nitabasamu au nionekane mzito kidogo? Nivae nini? Niseme nini ? Maswali haya yote yatajibiwa kwa wakati ufaao. Lakini jambo moja ni hakika: Haijalishi nitajiinua kiasi gani, bado nitakuwa mimi - Rachel. Rachel mdadisi, Rachel mwoga, na Rachel mtoto wa Mungu.

> **MAWAZO YA SIKU**
> Yote ambayo Mungu anaumba yanastahili sifa yangu.

Wakati Mungu anaponiangalia, Mungu haoni udhaifu wangu wote lakini huona mtu aliyeumbwa na vipaji na uwezo tata. Zaburi 139:13-14 inasema, *"Wewe umeniumba, mwili wangu wote; ulinitengeneza tumboni mwa mama yangu. Nakusifu maana nimefanywa kwa namna ya ajabu, matendo yako ni ya ajabu; wewe wanijua kabisakabisa."* Mungu anafikiri sisi ni wazuri bila kujali wengine wanaweza kufikiria nini.

Wakati tunaangalia kwenye kioo, tunaweza kukumbuka kwamba tunaona picha-kamilifu sanaa ya Mungu.

***Maombi:*** Mungu mpendwa, utukumbushe kwamba sisi ni kazi za mikono zako, na utusamehe wakati tunapokosa kuona uzuri wa kipekee ndani yetu na wengine. Amina.

**Rachel E. Dancy (Michigan, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE AMBAO WANA PICHA MBAYA YA KIBINAFSI**

**Swali la kujiuliza:** Ni nani au ni nini kina kukumbusha kwamba wewe ni kiumbe mpendwa wa Mungu ? Wakati unapojitayarisha kwa Conférence Générale namna gani utawasaidia wengine kukumbuka kwamba nao pia ni wa thamani kwa Mungu?

**SIKU YA KWANZA**
**08/04/2024**

# KATIKA DHORUBA

**Soma Mathayo 8:23-27**

***Basi, usiogope, mimi nipo pamoja nawe. Usifadhaike, mimi ni Mungu wako. Nitakuimarisha na kukusaidia; nitakulinda kwa mkono wangu wa ushindi.***

**— Isaya 41:10 BHN**

Nilikuwa na umri wa mwaka mmoja tu wakati familia yangu ilipohama kutoka Mashariki ya Pakistan (sasa ni Bangladesh) kwenda Magharibi ya Bengal, inchi ya India. Tukiwa wakimbizi, tuliishi katika hema lililotolewa na serikali kwa zaidi ya miaka saba. Nakumbuka jioni moja ya kiangazi chenye joto kali dhoruba kali ilikuwa ikitokea. Tulikuwa tuko na cheza kwenye kiwanja na dada yangu mkubwa akawa na wasiwasi na kuturudisha kwenye hema letu kwa usalama.

> **Mawazo ya Siku**
> Yesu yuko pamoja nami katika kila dhoruba

Mara tuliporudi, mpepo ulikuwa mkari sana hivi kwamba tuliogopa kupoteza hema letu na mali zetu zote. Nikiwazia jinsi tutakavyopoteza hema letu na kukosa mahali pa kuishi, nilianza kuomba Mungu. Nilihisi kwamba maombi yangu hayafanyi kazi. Kisha nilianza kuzungumza na Yesu. Nilianza kumsihi Yesu: Hatuna hema nyingine. Ikiwa huyu imekwenda, tutaishi wapi? Nilikuwa kwenye kona ya hema yetu niki shikilia kamba wakati, Nilisema nguvu “Nisaidie, Yesu!” Kwa mshangao wangu, mpepo ulitulia polepole na mwishowe imepita.

Uzoefu huu umekuwa na athari ya kudumu katika maisha yangu. Mungu ana tusikia wakati tunapo omba msaada. Kweli Yesu iko pamoja nasi katika kila dhoruba.

***Maombi:*** Mungu mpendwa, asante kwa kuwa nasi hata tunapopita wa kati ya nguvu ya maisha. Katika jina la Yesu. Amina.

**Subodh C. Mondal (Delhi, India)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WAKIMBIZI**

**Swali la kujiuliza:** Wakati maombi zako zinapaonekana kutojibiwa, ni nini inakusukuma kuendelea kuomba?

# WATU KUMI WALIOMBA

**SIKU YA PILI**
**09/04/2024**

**Soma 1 Wakorintho 12:12-20**

***Hawa wote waliendelea kujifunza kutoka kwa mitume, kuishi pamoja kindugu, kumega mkate na kusali.***

**— Matendo 2:42 BHN**

Miaka michache iliyopita, nilihisi kama kuna kitu kinakosekana katika maisha yangu. Masiku zangu zilikosa maana na kusudi. Hata hivyo, badala ya kumuletea Mungu mahangaiko yangu, nilitazamia utimizo katika sehemu nyingi zisizofaa—jambo ambalo lilinifanya najihisi mnyonge. Lakini nilijaribu kubadili njia zangu na kumgeukia Mungu.

Kundi langu la kanisa lilikuwa likilenga afya ya kiroho na liliwahimiza washiriki kushiriki mapambano yao. Ku mwanzo nilisita kuzungumzia juu ya utupu wangu. Watu wengi wanathamini nguvu, uhuru, na mafanikio, sio udhaifu au hitaji. Lakini ku mwisho nilifungua kwa kundi na nina omba msaada.

Baada ya mkutano huu, watu kumi walianza kuniombea. Muda mfupi baadaye, nilihisi uwepo wa Mungu na nguvu katika hali zilizojizunguka, zikinielekeza mbali na vikengeushi. Mahubiri, ibada, na maandiko ya Biblia ili nikumbusha juu ya utoaji wa Mungu. Mambo hayo kwa pamoja yalinisaidia kumtegemea Mungu.

Kuwa katika mazingira magumu haikuwa rahisi. Lakini nilipouliza, nikipata kwamba wengine walifurahi kusaidia. Washiriki wa kikundi walinitembelea mara kwa mara na kunitia moyo. Maombi yao na majibu ya Mungu yalinipa tumaini kwamba Mungu angenipa kusudi mupya na ata nipa kile ambacho kilikosekana katika maisha yangu.

**Mawazo ya Siku**
Wakati mnatafuta msaada, nita omba kwa wengine.

***Maombi:*** Asante, Mungu, kwa kujibu maombi ya familia yetu ya kanisa. Utusaidie kuomba msaada tunapohitaji. Amina.

**Jennifer Kirsch (Ohio, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **VIKUNDI VYA KANISA**

**Swali la kujiuliza:** Kumbuka wakati ambapo maombi yalifanya mabadiliko kubwa katika maisha yako. Namna gani uta ingisha maombi katika muda wako kwenye Conférence Générale?

SIKU YA TATU
10/04/2024

# UNA UHAKIKA, BWANA?

**Soma Yohane 4:4-24**

***Mungu yumo mjini humo, nao hauwezi kutikiswa; Mungu ataupa msaada alfajiri na mapema.***

**— Zaburi 46:5. BHN**

Ninakumbuka simu kama ilivyokuwa jana. Nyumba yangu ilikuwa ime jaa na kufulia kila mahali na vyombo vilivyohitaji kupangwa. Mtoto yangu moja mwanamke aka sirika na akakata simu. Hata mbwa hakufurahishwa nami ile siku. Nilikuwa najiona kama nimeshindwa.

**Mawazo ya Siku**
Mungu ananijua na ananipenda hata hivyo.

Viongozi wa kanisa wali nita ku simu na waka niuliza kama ningekuwa tayari kutumika kama kiongozi wa walei wa region kwa miaka minne ijayo. Nika jibu, " una uhakika unataka nifanye iyo kazi?" Wakati huo, siku ona vile maisha yangu inawezekana, na si kidioni kutumika kazi kubwa vile. Jinsi ilivyokuwa na nguvu kwangu kujua kwamba, kwa jinsi nilivyokuwa mchafuko, walimwona Mungu akifanya kazi maishani mwangu. Nilifikiriwa juu ya mwanamke kisimani na jinsi watu wengi hawagetaka awe mfano wa Kristo. Hata hivyo, anawakilisha kikamilifu sisi tunaomfuata Kristo.

Ikiwa tunataka kunenepesha kanisa na kuleta mioyo kwa Kristo, tunahitaji kuamini kwamba mioyo yote inastahili. Tunahitaji kuamini kwamba mioyo yetu inastahili kushiriki tumaini la upendo wake pamoja na wengine. Baada ya mwaka mmoja katika huduma, sijaribu kuficha maisha yangu ya fujo na yasiyo kamilifu. Nina kuwa uwazi na wengine. Nataka wale ambao wanahangaika wajue kwamba hawako peke yao. Tuko katika hili pamoja na Kristo.

***Maombi:*** Mungu mwenye rehema na upendo, tusaidie ku kufuata unapotuongoza kwa unyenyekevu na uaminifu ili wengine wajue kwamba imani ni safari yetu wote. Amina.

**Kimberly Rice Smith (North Carolina, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE WANAOJIONA HAWAFAI**

**Swali la kujiuliza:** Unauona wapi Mungu akifanya kazi katika ya Kanisa Méthodiste Unie? Namna gani umeitwa kumtumikia Mungu wakati huu?

**SIKU YA INE**
**11/04/2024**

# ZAWADI NDOGO

**Soma Luka 11:1-13**

***Kila kipaji chema na kila zawadi kamilifu hutoka mbinguni; hutoka kwa Baba, Muumba wa mianga, ambaye habadiliki wala hana alama yoyote ya ugeugeu.***

**— Yakobo 1:17 BHN**

Wakati nilipostaafu, nilipewa mto mdogo wa mviringo, wa kushonwa mikono. Niliiweka kwenye kiti, sawa decoration. Lakini, hivi karibuni mto huo imekuwa muhimu kwangu kila siku.

Kwa miezi miwili iliyopita nimekuwa nikipata nafuu kutokana kwa upasuaji ya uti ya mgongo. Usingizi umekuwa mgumu juu ya kidonda mu mgongo wangu. Wakati daktari aka ni ongoza ku weka mto katikati ya magoti yangu wakati ya kulala, nikikumbuka zawadi ya ile mto kidogo na nikaanza kuitumia nilivyoelekezwa. Wazia furaha yangu kupata kwamba mto huo ulinisaidia kulala bila maumivu!

Mungu wetu wa mapendo anatupatia zawadi kila siku – zawadi ambazo mara nyingi hatu juwe, ao atu tumikiye. Lakini Biblia imejaa mifano ya Mungu wetu anayejali akiwapa zawadi watu wengi sana—mfano bora zaidi ni zawadi ya Mwana wa Mungu, Yesu Kristo! Zawadi ya mto

> **Mawazo ya Siku**
> Zawadi kani Mungu amenipa leo?

***Maombi*** : Mungu mwenye upendo, aksante kwa zawadi ya Yesu Kristo na karama nyingi unazotoa kila siku. Amina.

**Roland Rink (Gauteng, South Africa)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE WANAOPATA NAFUU KUTOKANA NA UPASUAJI**

**Swali la kujiuliza:** Unaoneshaje shukrani kwa ajili ya zawadi ambazo Mungu amekupa?

**SIKU YA TANO**
**12/04/2024**

# MIKONO NA MIGUU

**Soma Mathayo 25:31-40**

***Mfalme atawajibu, 'Kweli nawaambieni, kila kitu mlichomtendea mmojawapo wa hawa ndugu zangu wadogo, mlinitendea mimi."***

**— Mathayo 25:40 BHN**

Maandiko ya leo ina maana mingi sana kwangu. Mstari hii ilinisaidia kutambua kwamba Yesu anataka tuwe mikono na miguu yake.

Nimepata maana mingi ya kumheshimu Kristo kupitia matendo ya huduma. Miaka kadhaa nyuma, nilianza kumtembelea mwanamke mwenye umri miaka 94 katika hospice ya wazee kila Jumatano.

> **Mawazo ya Siku**
> Leo naweza kuwa mikono na miguu ya Kristo.

Nilipata shangwe kumsikia akiongea kuhusu kupika kwenye kuni na kumbuka nyinginezo za enzi zake za ujana. Alikufa akiwa na miaka 96. Sasa ninasaidia na huduma ya chakula ya kanisa letu. Tunawapa chakual wale wanaohitaji na kutengeneza coffee kanisani Jumapili asubuhi. Ninafurayi ku kumbatia watu, na kusema, "Habari za asubuhi!"

Daima kuna hitaji ambalo linaweza kutimizwa. Unaweza kujitolea ku hospitalini, kuendesha gari kwa mtu kwa miadi ya muganga au kutuma kadi siku ya kuzaliwa kwa mshiriki wa kanisa. Hata kumfungulia mtu mlango inaweza kuwa njia ya kumutumikia Kristo. Tunawabariki wengine kwa tendo la huduma, na tunabarikiwa vilevile wakati tunapoheshimu Yesu na mikono na miguu yetu.

***Maombi*** : Mungu mpendwa, asante kwa kutu chagua kuwa mikono na miguu yako. Katika jina la Yesu, tunaomba. Amina.

**Roxie Ewing (Alabama, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE AMBAO WANA NJAA KATIKA JAMII YANGU**

**Swali la kujiuliza:** Kuwa mikono na miguu ya Kristo kunamaanisha nini kwako? Ni nani amekuwa mikono na miguu ya Kristo kwa ajili yako?

# KUKUBALIKA

**SIKU YA POSHO**
**13/04/2024**

**Soma Yohane 8:1-11**

***Yesu alipoinuka akamwuliza huyo mwanamke, "Wako wapi wale watu? Je, hakuna hata mmoja aliyekuhukumu?" Huyo mwanamke akamjibu, "Bwana, hakuna hata mmoja!" Naye Yesu akamwambia, "Wala mimi sikuhukumu. Nenda zako; na tangu sasa usitende dhambi tena."***

**— Yohane 8:10-11 BHN**

Huduma ya Yesu inatupa changamoto tuwakubali watu licha ya udhaifu na mapungufu yao. Wakati Yesu alipoanza huduma yake, alikutana na watu wa maina mbalimbali. Wengi Walimpenda yeye na mafundisho yake, lakini wengine hawakukubali yeye au mafundisho yake.

Wakati mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi alipoletwa mbele yake, Yesu hakumhukumu. Yesu hakumkwepa wala hakumdharau. Yesu hakumchukia. Yesu alifanya jambo ambalo halikutarajiwa. Alimkubali mwanamke hata kwa zambi zake na hali ya kijamii.

Bila kujali makosa na zambi zetu, sisi wote tunahitaji kukubalika. Yesu anatuonesha kwamba kukubali kunawezekana hata wakati watu wanatofautiana. Tunaweza kutoa zawadi ya Tunaweza kutoa zawadi ya kukubalika kwa wengine kwa sababu Mungu ametukubali.

**Mawazo ya Siku**
Nina fuata mfano wa Yesu wakati ninapo kubali wengine.

***Maombi:*** Mungu Baba, asante kwa kutukubali. Tafadhali tusaidie kukubali wengine. Amina.

**Golda Dilema (Cavite, Philippines)**

***Kusudi ya Maombi:*** **MTU AMBAYO NIMEMTENGA.**

**Swali la kujiuliza:** Ni wakati gani umepokea zawadi ya kukubalika kutoka kwa mtu fulani? Imefanya tofauti gani katika maisha yako?

SIKU YA JUMA
14/04/2024

# JESHI LA WASAIDIZI

**Soma 1 Yohane 3:16-18**

***Saidianeni kubeba mizigo yenu na hivyo mtatimiza sheria ya Kristo.***

**— Wagalatia 6:2 BHN**

Miaka mingi iliyopita, rafiki wa familia na ndugu katika Kristo alikuwa na cancer ya koloni ya stage 4. Kulikuja na wasiwasi mwingi. Rafiki yetu ndiye alikuwa na tumika, wa kati ngapi aliweza kufanya kazi kwa kusaidia familia yake? Ilikuwa ni wakati kuogofya.

> **Mawazo ya Siku**
> Ninaonesha mapendo ya Mungu wakati nina chugua mizigo ya wengine.

Mutume Paulo alishauri kanisa la Galatia kubebeana mizigo. Kupitia mambo ya muda mrefu ya rafiki yetu na saratani, Mungu alini fundisha mimi na wengine maana ya kweli ya maneno ya Paulo. Kubeba mizigo ya mwingine, ina lomba kutowa kintu fulani, ikiwe wakati, nguvu au pesa. Wa familia wengine waliunganisha pesa ili kulipa nyumba na bili za rafiki yetu. Wengine walitoa pesa juu ya chakula. Na wengine walijitolea kumpeleka na kurudi kwenye miada ya dactari (chimiothérapie). Jeshi la kweli la wasaidizi ilibeba mizigo ya familia hii. Zaidi ya yote, tulikuwa katika maombi ya kudumu kwa ajili ya uponyaji ya rafiki yetu.

Tulifunda kwamba wakati Mungu anapotuita kubebeana mizigo, aina asema tubebe mizigo yote peke yetu, lakini ni bebe ile mizigo kipande nilipewa. Kipande kiangu kinaweza kisionekane kama kipande yako.

Lakini kama kila mtu anabeba mizigo yake, basi itapunguza mizigo mnene. Katika kubeba mizigo ya wengine, tunatimiza sheria ya Kristo - kupendana kama vile Mungu alivyo tupenda sisi.

***Maombi:*** Yesu mupendwa, tufundishe jinsi ya kupenda wengine kama unavyotupenda sisi. Utusaidie kubeba mizigo ya wengine kwa huruma. Amina.

**Daphne Goodman (Maryland, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE WALIOGOFULIWA NA SARATANI**

**Swali la kujiuliza:** Itakuwaje kuchukuliana mizigo wakati wa Conférence Générale? Unawezaje kuwasaidia wengine katika majuma zijazo?

# MAHALI SALAMA

**SIKU YA KWANZA**
**15/04/2024**

**SOMA Zaburi 138:1-8**

***Akiniita, mimi nitamwitikia; akiwa taabuni nitakuwa naye; nitamwokoa na kumpa heshima.***

**— Zaburi 91:15 BHN**

Katika miaka ya 1950 nilisoma ku shule ya wanaume. Iliendesha kwa mtindo ya kijeshi  kwa discipline kali na adhabu ambayo mara nyingi zilitolewa mbaya. Uonevu shuleni ulikuwa umeenea na uliendelea. Bila shaka, mili teseka shuleni na kujifunza jinsi ya kuepuka ukonvi, na kutokujulikana wakati inahitajika.

Fazi moja katika shule ambayo hakuna mtu aliendа wakati mchana ilikuwa kanisa (chapel). Huko nilipata mafungo yangu ambapo faraja na msaada vilinіngoja. Nilifunza kwamba siku kuwe peke yangu. Nilihisi uwepo wa Mungu wenye kutia moyo, na nilifurahia uvutano huo wenye kutuliza na utegemezo. Huu ulikuwa mwanzo wa safari yangu ya maisha na Mungu.

**MAWAZO YA SIKU**
Katika Mungu, ninaweza kupata amani, uhakikisho, na ulinzi.

Nime endelea ku mshukuru Mungu kwa kuwa maishani mwangu. Siwezi kutoa shukrani kwa uzoefu ya kunioneya, lakini nashukuru kwamba wakati ile nilimpata Mungu. Maisha yangu yangekuwaje bila utangulizi huo mtakatifu?

***Maombi:*** Mungu wa mapendo, tafadhali safisha mioyo na akili za wale wanaowadhulumu wengine. Uwe pamoja na wale wanao kabiliwa na mateso, na utujalie maisha ya maelewano na amani. Amina.

**Johannes von Buch (United Kingdom)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WAATHIRIWA NA WAHALIFU WA UONEVU**

**Swali la kujiuliza:** Unaenda wapi kukutana na Mungu? Utaunganaje na Mungu ili kukufariji na kukutegemeza wakati wa Conférence Générale?

**SIKU YA PILI**
**16/04/2024**

# ZAWADI YA MUNKANA

**Soma Mathayo 28:18-20**

***Nami nipo pamoja nanyi siku zote; naam, mpaka mwisho wa nyakati."***

**— Mathayo 28:20 BHN**

Munkana wangu alinishangaza kwa zawadi ya Noeli, picha ya kushonewa yenye ina soma, " Mimi Nipo Pamoja Nanyi Siku zote,? Mathayo 28:20." Hasikujue maana ambao ile mstari ya Biblia ilikuwa nao kwangu miaka mingi iliyopita.

Wakati ni lipokuja Marekani miaka 66 iliyopita, nilizungumza Kiingereza kidogo. Nilijiunga na kikundi cha vijana katika kanisa langu, kikiongozwa na kijana mwanafunzi. Muda si muda aliona kwamba nilikuwa nimejitenga kabisa. Lakini baada ya maneno kidogo, nikafunguka na kumwambia niko na magumu ya kuendelea na masomo yangu. Kisha akataya Mathayo 28:20. Aka niambia kwamba Yesu alikuwa akizungumza nami na kwamba alikuwa pamoja nami kila wakati katika kila hali. Nika sikiya nguvu na Imani yangu ikapanda. Kuanzia siku hiyo nilifurahi zaidi na kufunguka kwa marafiki shuleni.. Nilipojitayarisha examen ama projet fulani, nilijua nilijua sikuwa peke yangu - Yesu angekuwa nami.

**Mawazo ya Siku**
Maneno na matendo yangu yanaonyesha je imani yangu kwa Mungu?

Baada ya kukumbuka hizi, nilimpigia simu munkana yangu na ni kamwelezeya maana ya mstari hio maishani mwangu. Zaidi nili ongeya naye mabadiliko ahadi ya Yesu inaleta katika maisha yangu.

***Maombi:*** Baba mpendwa, asante kwa kututumia Yesu. Tuonyeshe njia za kuhudumia marafiki na familia zetu na kuwaonyesha zawadi yako ya upendo na neema. Amina.

**Elli Morawietz (Florida, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WA KAMBO NA WANKANA**

**Swali la kujiuliza:** Kuwa pamoja na Yesu kunakupa je ujasiri na nguvu kwa majuma zijazo?

# IMETIA NANGA

**SIKU YA TATU**
**17/04/2024**

**Soma Zaburi 46:1-11**

***Tunalo tumaini hilo kama nanga ya maisha yetu.***
**— Waebrania 6:19 BHN**

Mimi na mume wangu Mike tulienda kutembea mu muji wa karibu ili tuchinguze macho yetu. Wakati tulikuwa na tazama fremu mpya za miwani ya macho Mike akaanguka, akigonga kichwa chake chini. . Hata kama alishtuka waziwazi, alikuwa na kivimbo kubwa kichwani mwake. Tuliita gari la wagonjwa na kuelekea hospitalini.

Tukiwa tunangoja kwenye korido iliyokuwa na watu wengi, nilijikuta nikajiuliza Mungu yuko wapi. Kwa nini hii ilikuwa imetokea? Ni uharibifu gani ulifanyika? Kama ninge sikiya amani ya Mungu badala ya kuzikiya mkazo.

Kisha nimekumbuka kintu moja kutoka ibada nilisoma asubuhi hiyo. Sikuwezi kukumbuka maelezo mengi; lakini nilijua ilikuwa kitu kuhusu nanga: jinsi Mtakatifu Paulo alikuwa alivurugwa baharini na jinsi Mungu anavyotuchunga salama katika dhoruba za maisha.

Nilihisi kwamba Mungu alikuwa akiniambia, "Nimekupata." Umetia nanga." Niliendelea kujirudia huku nikisubiri kwa hamu hospitalini. Sikuhisi mng'aro wa amani, lakini nilijua kwamba tulikuwa mikononi mwa Mungu. Tulitia nanga.

Na Mike alikuwa na yuko sawa. Ninatoa shukrani kwa uaminifu wa Mungu na kwa neno la Mungu ambalo bado linazungumza nasi leo.

**Mawazo ya Siku**
Ninasimama katika upendo wa Mungu.

***Maombi:*** Asante Mungu mwaminifu, kwamba wakati mambo za maisha zinatenkesha salama yetu wewe unatushikilia na usituachie kamwe. Amina.

**April McIntyre (England, United Kingdom)**

***Kusudi ya Maombi:*** **MTU ANAYEPONA KUTOKANA NA ANGUKO**

**Swali la kujiuliza:** Ni andiko gani au mazoea gani ya kiroho inakusaidia kukaa imara katika Mungu katika wakati wa magumu?

SIKU YA INE
18/04/2024

# KUPUNGA MKONO KWENYE DIRISHA

**Soma Ufunuo 3:14-21**

***Sikiliza! Mimi nasimama mlangoni na kubisha hodi.***

**— Ufunuo 3:20 BHN**

Sikuzote nilikuwa na kazi la kuwaacha watoto wetu kwenye shule la watoto, jambo ambalo ni gumu zaidi kuliko kazi la mume wangu la kuwachukua. Watoto wangu hawakupenda kuachwa, na asubuhi nyingi zilijaa machozi. Pia haikusaidia kwamba shule ilikuwa mahali sana na fazi nilipofanya kazi, kwa hivyo bila shaka nilikuwa na haraka kila mara.

**Mawazo ya Siku**
Nitatafuta mwangaza wa upendo wa Mungu kwangu leo.

Asubuhi moja, nilikuwa nikitoka nje ya shule la watoto kwa haraka hadi kwenye gari langu, wakati kitu fulani kilinivutia. Katika dirisha linalotazama sehemu ya kuegesha magari, mwanangu wa miaka miwili alisimama akini pepeya mkono kwa furaha. Ilikuwa tamu sana na kile nilichohitaji. Nilimwambia kila mtu kazini jinsi mwanangu alivyokuwa mtamu.

Asubuhi iliyofuata, wakati nilimpeleka mtoto yangu, nilimtaja mwalimu jinsi mwanangu alivyonifanya siku iliyopita. Aliniambia kwa fadhili kwamba yeye hufanya hivyo kila asubuhi na amekuwa akifanya hivyo kwa miezi mingi. Moyo wangu ulifadhaika. Sikuwahi kukosa kuona mtoto aka ni pepeya baada ya hapo.

Experience hili lilinifanya nijiulize ni mara ngapi nimekosa ishara za upendo wa Mungu kwa sababu niliharakishwa kuona. Bwana asifiwe tunapendwa na Mungu mvumilivu na upendo wake hauna mwisho.

***Maombi:*** Mungu mpendwa, utusamehe wakati hatuoni namna zote unaotupenda. Asante kwa kutuchunga na kwa kutupenda bila mwisho. Amina.

**Rebekah L. Callen (Texas, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **SHUKRANI KWA UPENDO WA MUNGU**

**Swali la kujiuliza:** Utachukua muda gani kutulia na kutafuta ishara za upendo wa Mungu wakati wa Conférence Générale?

# KUMSIKILIZA MUNGU

**SIKU YA TANO**
**19/04/2024**

**Soma 1 Petro 5:1-10**

***Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa enzi wa Mungu, ili awainue wakati ufaao. Mwekeeni matatizo yenu yote, maana yeye anawatunzeni.***

**— 1 Petro 5:6-7 BHN**

Nilikuwa na kazi nzuri, familia, na nyumba mu fazi nzuri. Kisha nikachana na muke wangu, na kila kitu kilibadilika. Kuishi ndani ya gari langu kwenye barabara yenye kelele, nikilala na blanketi juu ya kichwa changu ili kuzuia baridi na nisione mwanga, na kula peke yangu nje katika benchi ilinilazimu kutafakari na kumsikiliza Mungu.

Nilikaribishwa na wengine wasiyo na nyumba, na kukubalika kwao kulinisaidia kuona kwamba Mungu yu ndani ya kila mtu. Ukosefu wa makao ulikuwa unyenyekevu, lakini Yesu alijinyenyekeza kwa ajili yetu. Tumeitwa kutembea kwa unyenyekevu na Mungu, kama Yesu alivyofanya alipokuwa njiani kuelekea Msalabani. Mungu aliniinua, akinifundisha kumpelekea msigo langu, kumwona Mungu katika asili, kuthamini kila mtu, na kuacha maisha yangu mikononi mwake.

Mungu alinielekeza kwa kanisa ambayo imenisaidia kukua katika imani, ambapo ninafanya kazi katika misheni ya uenezi, ikiwa ni pamoja na wale ambao hawana makao. Usaidizi wa watu katika kanisa hii ilifanya iwe rahisi kufuata njia ya Mungu. Mungu anatuita kuwalisha wenye njaa, kuwatembelea wagonjwa, kuwakaribisha wageni, na kuwajali wasio na nyumba…sikiliza.

**Mawazo ya Siku**
Mungu uniongoze katika kila hali ili kunisaidia kufika mwito wangu.

***Maombi:*** Fungua macho na mioyo yetu, Ee Mungu, kwa mahitaji ya wale wanaotuzunguka. Fungua masikio yetu ili kusikiliza maongozi yako. Amina.

**Brian Rogers (Massachusetts, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE WASIO NA NYUMBA**

**Swali la kujiuliza:** Inamaanisha nini kwako kutembea kwa unyenyekevu pamoja na Mungu? Unafanyaje mazoezi haya katika maisha yako ya kila siku?

**SIKU YA POSHO**
**20/04/2024**

# NGUVU YA CHUMVI

**Soma Wakolosai 4:2-6**

***Mazungumzo yenu yanapaswa kuwa daima mema na yaliyokolezwa kwa chumvi na ya kuvutia, na mnapaswa kujua jinsi ya kumjibu vizuri kila mmoja.***

**— Wakolosai 4:6 BHN**

Baadhi ya familia katika kanisa letu zinazoishi katika mahali fulani ambapo wana kikundi cha ushirika. Tunakutana kila mwezi kwa ajili ya kujifunza Biblia, maombi, na kupata manufaa ya familia zetu. Ni wakati wa ushirika na ujenga. Daima tunaleta chakula ili kushiriki. Pindi moja nilipika kari ya kuku. Nilisubiri kupokea maoni mazuri kwa chakula, lakini hakuna mtu aliyesema kintu. Mwisho yake, niliuliza ikiwa walipenda sahani. Walitazamana bila kunijibu. Nikiwa nashangaa kwa nini, nilichukua kijiko ili kuonja. Kwa mshangao niligundua kuwa nlikuwa nimesahau kuongeza chumvi!

**Mawazo ya Siku**
Yesu anataka nilete upendo na nuru ya Mungu duniani.

Nilikumbushwa maneno ya Yesu katika Mathayo 5:13, *Nyinyi ni chumvi ya dunia. Lakini chumvi ikipoteza ladha yake itakolezwa na nini? Haifai kitu tena, ila hutupwa nje na kukanyagwa na watu.* Kama chumvi ya dunia, tunafanya kazi ya kuhifadhi kila lililo jema na la haki duniani kwa kuwa wapatanishi na walinda amani. Kama vile chumvi huongeza ladha ya chakula, kama Wakristo tunaweza kuleta upendo, wema, na neema kwa wale wanaotuzunguka kwa kushirikiana na Mungu, tukiakisi upendo na nuru ya Mungu ulimwenguni.

***Maombi*** : Mungu mwenye mapendo, tunatamani kukutumikia wewe. Tusaidie kujenga mahali yenye haki na amani ambapo tunaonyesha upendo wako na huruma kwa wale wanaotuzunguka. Amina.

**Navamani Peter (Karnataka, India)**

***Kusudi ya Maombi:*** **MAJIRANI ZANGU**

**Swali la kujiuliza:** Yesu alisema, “Ninyi ni chumvi ya dunia.” Je, ungependa kuona Kanisa Méthodiste Unie likiishi hivi?

# KUOMBA KWA UJASIRI

**SIKU YA JUMA**
**21/04/2024**

**SOMA Mathayo 18:1-5**

***Kisha akasema, "Nawaambieni kweli, msipogeuka na kuwa kama watoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni.***

**— Mathayo 18:3 BHN**

Binti yetu mdogo alilala kitandani, akifunika hadi mbanga. Baada ya wimbo, nilimuuliza swali ile tunalo uliza kila jioni: "Unataka kuombea nini?"

Alinyamaza, midomo ikishikana, mu mawazo. Alijibu, "Nataka kumwomba Mungu afanye nyati (Licorne) ikuwe kweli.

Katika ugumu wa maisha ya kila siku, si ngumu kupoteza imani yetu, ya kuamini na yenye macho. Lakini kuhusu watoto, kwa nini wasimwombe Mungu chochote? Ikiwa Mungu anaweza kuponya wagonjwa, kufufua wafu, na kuumba sayari katika anga ya juu, hakika Mungu anaweza kufanya nyati (licorne) ikuwe halisi! Na ikiwa binti yangu ana imani ya kutosha ombi kame hilo, ninataka imani kama ya kitoto kumwomba Mungu mambo makubwa na ya ujasiri pia.

> **MAWAZO YA SIKU**
> Leo nitaomba kwa ujasiri.

Sisi zote tunapitia nyakati ambapo imani yetu inahisi kuwa ndogo, wakati hatujathubutu kutumaini kwamba Mungu anaweza kuleta uponyaji au upatanisho au utimilifu. Hata hivyo, Mungu bado ni Mungu wa yasiyowezekana. Kwa hiyo, tuchukue ukurasa kutoka kwa watoto kati yetu na kuanza kumwomba Mungu kwa mambo makubwa, yanayoonekana kuwa haiwezekani.

***Maombi:*** Mungu mpendwa, itia mioyo yetu yenye mashaka ikuamini kwa imani kama ya kitoto. Utupe ujasiri wa kuomba kwa ujasiri. Kwa jina la Yesu. Amina!

**Gretchen Schloesser (Arizona, USA)**

***Kusudi ya Maombi:*** **KUKOMESHA IMANI KAMA YA MTOTO**

**Swali la kujiuliza:** Ni maombi gani makubwa, ya ujasiri utaomba kwa ajili ya Conférence Générale?

SIKU YA KWANZA
22/04/2024

# AJABU YA NYOTA

**Soma Zaburi 19:1-4**

***Mbingu zatangaza utukufu wa Mungu; anga ladhihirisha kazi ya mikono yake.***

**— Zaburi 19:1 BHN**

Miaka nyingi iliyopita, mimi na mke wangu tulikaa katika jumba kwenye Milima mu Rocky Mountains. Sitasahau usiku huo. Mbingu ilijaa mamilioni ya nyota nzuri. Walionekana karibu sana hivi kwamba tungeweza karibu kuwafikia na kuwagusa. Tuli watazama kwa muda, tukimsifu na kumwabudu Mungu wetu mkuu kwa maajabu ya uumbaji.

**Mawazo ya Siku**
Uzuri wa uumbaji wa Mungu uko karibu nami.

Maneno ya Zaburi 19:1-4 yalikuwa wazi kwetu jioni hiyo: Mbingu zatangaza utukufu wa Mungu; anga ladhihirisha kazi ya mikono yake. Mchana waupasha habari mchana ufuatao, usiku waufahamisha usiku ufuatao. Hamna msemo au maneno yanayotumika; wala hakuna sauti inayosikika; hata hivyo, sauti yao yaenea duniani kote, na maneno yao yafika kingo za ulimwengu. Mungu ameliwekea jua makao yake angani.

Viumbe vyote vinasema na nguvu juu ya Mungu - hekima isiyo na kikomo ya Mungu, ukuu, na nguvu za uumbaji. Popote pale tunaishi, tunaweza kutazama pembeni na kuona ajabu na uzuri ya uumbaji ya Mungu.

***Maombi:*** Mungu wa ajabu, fungua macho yetu tuoni ajabu na utukufu wa uumbaji wako. Amina.

**Hank DeGraaff (Michigan, USA)**

***Kusudi wa Maombi:*** **SIFA KWA UZURI WA UUMBAJI**

**Swali la kujiuliza:** Utachukuaje wakati ili kushuhudia utukufu wa uumbaji wa Mungu katika majuma yanayokuja?

# HATA HIVYO, SI KWA SABABU

**SIKU YA PILI**
**23/04/2024**

**Soma 1 Wathesalonike 5:12-16**

***Na kuwa na shukrani katika kila hali. Hayo ndiyo anayotaka Mungu kwenu katika kuungana kwenu na Kristo Yesu.***

**—1 Wathesalonike 5:18 BHN**

Mara nyingi nimesikia ikisemwa kwamba “Mungu hatatupa kamwe zaidi ya utwezavyo.” Walakini, kuna nyakati katika maisha yetu ambapo hii sio kweli, na taarifa kama hizo hazina maana. Pengine maandiko ya Biblia ilivyotumiwa kuunga hili imetafsiriwa vibaya. Kwa mfano, andiko la 1 Wakorintho 10:13 linatajwa kwa kawaida, lakini linasema majaribu badala ya kuteseka.

Vifungu kama 1 Wathesalonike 5:16-18 na Yakobo 1:2 vinatuambia tufurahi daima. Lakini kuambiwa tushangilie tunapofiwa na mpendwa wetu au tunakabiliwa na uchunguzi wa afya unaobadili maisha kunaweza kuonekana mabaya Amri ya kufurahia mateso yetu, hata hivyo, inahusu kufurahi katika Yesu licha ya hali zetu, si kwa sababu ya hali zetu. Uelewaji huo unaweza kuleta tofauti Iliyoje wakati majaribu yanapokuja! Ni rahisi sana kufurahi katika Yesu na yale ambayo ametufanyia kuliko kufurahia magumu tunayokabili.

> **Mawazo ya Siku**
> Macho yangu yanaelekezwa Mungu au mambo zangu?

Kuelewa vifungu hivi vyema kumenisaidia kuinua macho yangu kutoka kwa hali ngumu sana hadi kwa Mungu, ambaye yuko pamoja nasi kila hatua ya njia, akitoa tumaini, furaha, na kutia moyo katikati ya hali ngumu zaidi za maisha.

***Maombi*** : Baba wa Mbinguni, asante kwa kuwa pamoja nasi katika mateso yetu. Tusaidie kufurahi katika weye si kwa sababu ya hali zetu. Katika jina la Yesu tunaomba. Amina.

**Bronwyn Ashton Winch (Queensland, Australia)**

***Kusudi ya Maombi:*** **WALE WALIO KATIKA HALI YA KUHUZUNISHA MOYO**

**Swali la kujiuliza:** Wakati mambo yanapotokea, ni nini hukusaidia kushangilia na kumtegemea Mungu ili akupe tumaini na kitia-moyo?

## Baraka

Ombi langu ni kwamba masomo, mawazo na maombi yaliyotufikisha siku hii yametoa njia

ya maandalizi kwa ajili ya mkutano mtakatifu unaokuja. Tunapoanza wakati huu pamoja kama wa ndugu wa Kanisa kuu Méthodiste Unie, ninajawa na shukrani na matumaini. Ninaomba mkusanyiko wetu uwe ushuhuda wa nguvu zetu katika tofauti zetu na imani yetu.

Katika mawazo ya John Wesley, ambaye alitetea umoja katika utofauti, naomba tusikilize mazuri historia ya kila mmoja wetu, tushiriki furaha na huzuni zetu kwa huruma, na tupate msingi wa kawaida katika utume wetu wa kueneza upendo na neema ya Mungu wakati tunafanya kazi kufanya wanafunzi kwa mabadiliko ya ulimwengu.

Kusanyiko letu ni ukumbusho kwamba ata tunatoka katika tamaduni tofauti, tunazungumza lugha tofauti, na tunaweza kuwa na mitazamo tofauti, sisi zote ni mwili mmoja katika Yesu Kristo. Lakini umoja huu sio usawa; ni umoja unaosherehekea na kuheshimu tofauti zetu. Ninajua kwamba pamoja tuna nguvu zaidi na tunaakisi ufalme wa Mungu.

Wakati tunapounda nafasi takatifu pamoja ku pitia Roho Mtakatifu, tuendelee kutafuta ufahamu na uponyaji palipo na mgawanyiko, kutoa neema tunapoumizwa, na kumwilisha upendo ya Kristo ndani yetu. Ili kuonyesha hamu yetu ya kushikilia nafasi kwa ajili ya mtu mwingine, The Upper Room inatoa chumba cha maombi (Salle E222) katika mkutano hii ya Conférence Générale. Kikundi yetu iko hapa kutoa fasi ya kutafakari kwa utulivu na usaidizi wa maombi.

Amani ya Mungu iwe pamoja nasi, mapendo mtakatifu ituzunguke, na hekima ya Mungu itongozwe hapa kwenye Conférence Générale. Amina.

— Kimberly Orr
Mchapishaji
The Upper Room

## Mfano gani kuandika kwa The Upper Room

Ibada katika kila toleo ya kitabu ya méditations *The Upper Room* imeandikwa kwa watu kama wewe. Hapa kuna miongozo ya kukusaidia kuandika:

- Eleza jambo moja tu katika ibada.
- Ongeza maelezo ya kile ulichosikia, kuona, kuhisi, au kusema.
- Eleza historia yako mwenyewe na ukweli wa kiroho uliojifunza kutoka kwayo.
- Ongeza usomaji wa Biblia, maandiko, na maombi.

Tunafanya kazi mwaka mmoja kabla ya kuchapisha. Tukichagua kuchapisha ibada yako, tutakujulisha.

Tuma ibada zako kwa ureditorial@upperroom.org au **Submissions.UpperRoom.org**

Ibada bila maelezo ya mtumaji hayaitaangaliwa ili kuchapishwa.

## Kuhusu The Upper Room

The Upper Room® ni ministère inayojitolea kusaidia maisha ya kiroho ya Wakristo wanatafuta kumjua na kumwona Mungu kikamilifu zaidi.

Tangu mwanzo wake kama kitabu ya méditations, The Upper Room imekua kikijumuisha machapisho, programu, usaidizi ya maombi, na vitu vingi via kusaidia wakwamini wa kila miaka na kila dénomination kukomeya mu imani na huduma.Kazi ya kudumu na ya kiroho inaendelea kwa nguvu katika The Upper Room wakati tunapoalika watu kuishi maisha ya kila siku pamoja na Mungu.

Tangu 1935 The Upper Room imekuwa  na jiendesha kupitia mauzo, malipo ya washiriki , na zawadi kutoka kwa wafadhili. Una weza kujifunza zaidi kwenye **UpperRoom.org**.

## Nyenzo zingine za Maombi na Maandalizi

Kwa zaidi ya miaka 85, jumuiya ya kimataifa  imekusanyika kila siku kupitia kitabu ya méditations ya *The Upper Room*. Unaweza kujiandikisha kwa toleo la kuchapishwa au la dijitali kwa **UpperRoom.org/subscribe**.

Pata maelezo ya lugha ya Kiswahili ya *The Upper Room* katika **UpperRoom.org/international**.

Unaweza kutupata kwenye Conférence Générale au ku **UpperRoom.org/umc2024**